# Motifu ya Safari katika Kazi za M. S. Mohammed

*Evans Mbuthia*
*Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya*

**Ikisiri**

**M. S. Mohammed ni mwandishi maarufu katika fasihi ya Kiswahili. Kazi zake tatu ambazo zinamulikwa katika makala haya zinamtambulisha kama mwandishi ambaye ana mazoea ya kutumia mbinu ya safari ili kukuza maudhui yake. Wahusika wake wanapitia tajriba anuwai katika safari zao ambazo zinawapelekea kukua, kujitambua, kujinasua, kukengeuka na hata kuangamia. Katika kazi zake zilizoteuliwa: *Kiu*, *Nyota ya Rehema* na *Kicheko cha Ushindi*. Hali hizi zinajitokeza na kuwa kama funzo kwa wasomaji ambao wanashauriwa kuzingatia waendako na waendavyo. Ni bayana kwamba motifu ya safari ina nafasi muhimu katika kazi za M. S. Mohammed na makala haya yanazamia hilo suala kwa kina. Ili kuweka mambo bayana, makala haya yametumia Sosholojia ya Kifasihi kama kurunzi ya kumulika wanayoyapitia wahusika katika kazi zilizoteuliwa.**

**Maneno Muhimu:** Motifu, Sosholojia ya Kifasihi, Saikolojia, Hisia, Kutamauka, Mwamko.

## Utangulizi

Tofauti na waandishi wengi wa fasihi ya Kiswahili, M. S. Mohammed ni mwandishi ambaye si mwalimu. Hata hivyo vitabu vyake vitatu; riwaya mbili (*Nyota ya Rehema* na *Kiu*) pamoja na diwani yake ya hadithi fupi (*Kicheko cha Ushindi*) ni amana ambazo zina mafundisho mengi kwa wasomaji. Katika riwaya hizi, pamoja na baadhi ya hadithi katika diwani yake iliyoteuliwa, motifu ya safari ni mhimili muhimu mno katika ukuzaji wa kazi hizi. Ni kutokana na safari ambapo wahusika wake wanapata fursa ya kutagusana na asasi nyingi za kijamii na hata wanajamii tofauti, jambo linalowafanya kufunguliwa ulimwengu tofauti ambao unawaathiri ama kwa shari au heri.

Sosholojia ya fasihi ambayo imetumika katika kazi hii imetusaidia kuelewa kwa ukamilifu zaidi kuhusu athari ya mtagusano wa wahusika na jamii tofauti wanaposafiri ili kusaka wanayoyataka au kukimbia hali ambazo zinawaletea vizingiti katika maisha yao. Motifu ya safari huhusisha kuondoka, vizingiti vinavyomtatiza msafiri njiani na marejeo. Kila hatua ina umuhimu wake. Hatua ya kwanza haitokei bila tafakari inayomchochea mtu kusafiri. Hatua hii pia inaweza kuhusisha upangaji wa safari yenyewe. Maswali kama vile: je safari

itakuwa ya usiku au mchana? Ya siri au wazi? Na ni wapi kunakoendwa? Maswali haya sharti yajibiwe. Hatua ya pili inahusu kuwazia namna ya kutafuta nyenzo za kusafiri na mbinu za kukabiliana na vizingiti njiani. Mwisho, msafiri anaweza kujiuliza namna atakavyorejea kama italazimu.

Safari pia inaweza kuwa ya kisaikolojia na kihisia kwa lengo la kufikia matamanio fulani ambayo msafiri anayasaka. Safari ya sampuli hii ambayo husafirisha fikra kutoka hali moja hadi nyingine ndiyo hutoa shinikizo la safari halisi. Mathalani mhusika anaweza kukumbwa na matatizo mengi katika mazingira yake ambayo yanaweza kuibua mawazo mengi kuhusu namna ya kujinasua kutokana na hali hizo zinazomkera. Hatua hii inaweza kuisafirisha akili yake hadi mahali anapotamani na kumfanya apaone kwa macho yake ya kihisia. Mhusika pia anaweza kujipata katika hali inayomkengeusha na kufanya akili yake kusafiri hadi alikotoka ambapo anapaona patulivu. Aghalabu, hali hii huwakumba wasafiri wanaosafiri katika mataifa ya nje au miji mikubwa na kukumbana na mazingira mageni na mifumo tofauti ya kijamii. Katika kazi tulizozipitia, tulimulika safari za wahusika mbalimbali wakiwemo Rehema na Sulubu (katika *Nyota ya Rehema*), Idi na Rehema (katika *Kiu*) na Adamu na Mambo (katika *Kicheko cha Ushindi*). Je safari wanazofunga au kufungishwa zinawawezesha kuyafikia matamanio yao? Makala haya yanajadili suala hili na mengine.

## Msingi wa Kinadharia

Ili kufikia malengo ya makala haya, mwandishi ametumia nadharia ya Sosholojia ya kifasihi. Ufaaji wa nadharia hii unatokana na ukweli kwamba maisha ya kila mwanadamu ni kama uzi unaotumika katika ufumaji wa vazi la jamii. Hivyo, maisha ya kila mhusika kama yanavyowasilishwa katika kazi za kifasihi huchangia katika kuielewa jamii husika. Ukweli huu unaafikiana na maoni ya Wellek na Warren (1978:210) ya kwamba katika jamii mwanadamu hulazimika kuwa katika taasisi anuwai ambazo huwa kama "kalibu ambalo litaamua umbo lake". Kauli hii ya Wellek na mwenzake inashadidiwa na Witte (1978) anapoeleza kuwa: "Silika ya mwanadamu na maisha yake kwa ujumla huamuliwa au kudhibitiwa na jamii yake" (uk211). Kauli hii ni yenye mashiko na kuaminika kwa kuwa mwanadamu huishi katika jamii ambayo dira yake ni sheria rasmi zilizo kwenye katiba ya jamii husika au miko na sheria za kijamii ambazo kila mwanajamii husika hulazimika kuziheshimu. Kauli hii inatupeleka kwenye ufafanunzi waWamitila (2003):

> Wahakiki wa Kisholojia hushikila kuwa kazi ya kifasihi imedhibitiwa na muundo wa kijamii, kiuchumi na kisiasa pamoja na kani au nguvu za wakati fulani maalum. Kudhibitiwa huku kunajitokeza katika uteuzi na ukuzaji wa mada, jinsi ya uwazaji, inavyotathmini maisha na inavyowasilishwa na mtindo wake ( uk 204).

Katika makala haya, wahusika wanalazimika kufunga safari. Katika jamii wanamotoka walikuwa chini ya mamlaka rasmi za kiserikali na vilevile, kama mwanajamii yoyote yule wanakohama na wanakohamia watakumbana na hali tofauti japo watadhibitiwa na sheria fulani. Hatima ya maisha yaitategemea jinsi watakabiliana na hali badalia za kijamii watakozokabiliana nazo safarini na katika jamii zao mpya. Hatimaye watarejea iwapo wataweza kwa kuwa hata maangamizi na mauti huwakumba wasafiri.

Safari ni tendo ambalo haliepukiki katika maisha ya mwanadamu. Katika juhudi za kujiendeleza, mwanadamu anawajibika kusafiri ili kusaka anachokitaka au hata yeye mwenyewe kujisaka ili ajifahamu zaidi. Kutokana na hali hii, kuna waaandishi kadhaa ambao wametumia safari kama kiunzi kikuu cha kukuza kazi zao. Baadhi ya waandishi hawa ni kama vile Conrad (1910) anaposimulia kuhusu safari zake kwa kutumia meli. Safari ambazo zilimtoa kwao uzunguni na kumpeleka hadi Afrika. Safari hizi zinampa nafasi ya kuwa na mtagusano na watu weusi. Anayoyasema kuwahusu Waafrika ni dhihirisho kamili la chuki ya kimataifa. Anaeleza yafuatayo:

> Nakumbuka kwa mbali na kwa mshtuko, kama kupitia katika dunia ya ajabu ambayo haina matumaini wala matamanio.Nikajipata katika mji huo wa huzuni nikiwachukia raia waliokuwawakipita mbio mbio kuelekea katika shughuli za kuibiana hela kidogo ili wapatemtaji na kuweza kula chakula chao ovyo na kunywa pombeyaoduni na kuotandoto zao zisizo na maana.Wakahitilafiana na mawazo yangu.Walikuwa kama wavamizi ambao nina hakika hawakujua nilichokijua mimi (uk. 119).

Semzaba (1999) pia anatumia motifu ya safari kutekeleza malengo yake ya kidhamira. Katika Funke Bugebuge wahusika wake wakuu Bugebuge na Chambo wanaingia katika ushindaani wa kitabaka na kisiasa. Motifu ya safari inadhihirika katika viwango viwili. Kuna safari ya Chambo kutoka mjini. Anafunga safari hii ajikuze kiuchumi na hatimaye aingie kwenye ulingo wa kisiasa. Safari nyingine ni ya Bugebuge ya kupigana na ulitima kwa kushirki biashara ndogo ndogo. Safari yake ya kupambana na umaskini na kuutafuta umaarufu wa kisiasa inakumbwa na misukosuko mingi ambayo inafanya kazi hii kuwa na msuko wa kusisimua.

Muthoni (2014) alichunguza Mtindo ambapo anarejelea matukio katika riwaya hiyo. Tunaelezwa yaliyowapata wahusika wakuu katika safari zao. Zinji, Maya, Sapna na Kombo wanazuru miji mingi katika nchi ya Tikitimaji. Ziara zao zinakuwa ni za kiutambuzi na za kujitambua. Wanatambua chanzo cha matatizo yanayowakumba watu wa Tikitimaji na kuwapa nafasi ya ujitambuzi wa kibinafsi ambapo Sapna anagundua asili yake. Ni bayana kuwa Wamitila anatumia motifu ya safari kwa ufundi mkubwa katika kazi hii kama alivyofanya katika kazi zake nyingine. Silavwe (2016) anatufahamisha kuhusu masaibu mengi ambayo

Majaliwa alikumbana nayo katika juhudi zake za kutafuta marimba yake. Kupitia motifu ya safari, msomaji anajuzwa mengi kuhusu itikadi za jamii husika. Mugo (2016) alichunguza matatizo ya wanawake nyakati za ukolono nchini Kenya. Alikita kazi yake katika motifu ya safari na, kwa hivyo, anaifanya kazi yake kusisimua zaidi. Kuhusu utafiti wake alieleza:

> Utafiti huu unachunguza matumizi ya motifu ya safari kama mkakati unaotumiwa na wahusika wanawake kama njia mojawapo ya kutafuta ujitambuzi katika nyakati za ukoloni nchini Kenya. Hadithi ya Mulwa *Flee, Mama flee* (Toroka, Mama toroka) inaibua matatizo ambayo wenyeji waliyapitia nyakati za ukoloni hasa wanawake ambao pia walilazimika kukabiliana na viunzi vinavyotokana na jinsia yao kama wanawake (uk 3) (Tafsiri yetu).

Kwa hivyo ni bayana kuwa motifu ya safari ni mtindo wa kukuza maudhui ambao ni maarufu miongoni mwa baadhi ya waandishi. Mikakati hii husaidia uendelezaji bora wa maudhui na huibua msimamo wa mwandishi kuhusu masuala anuwai.

## Majadiliano kuhusu Motifu ya Safari katika Kazi za M. S. Mohammed

M. S. Mohammed amekita kazi zake nyingi katika motifu ya safari. Suala la safari linajitokeza karibu katika kazi zake zote. Ni kutokana na safari ambapo masuala anayoyajadili yanaibuka, kukuzwa na kupewa uhai. Hali hii inadhihirika katika kazi zinazochunguzwa katika makala haya. Kazi zenyewe ni riwaya mbili (*Nyota ya Rehema* na *Kiu)* na Hadithi mbili fupi *'Mji na 'Uhuru wa Siku Moja'(Kicheko cha Ushindi)* ambazo zimetungwa na kuhaririwa na M. S. Mohammed.

## Motifu ya Safari katika *Nyota ya Rehema, Kiu*, '*Mji'* na '*Uhuru wa Siku Moja'* (*Kicheko cha Ushindi*)

### *a) Nyota ya Rehema*

*Nyota ya Rehema* ni riwaya ambayo inazungumzia mahusiano ya kinyumba na hata ya kitabaka. Masuala mengine muhimu katika riwaya hii ni uozo wa kijamii unaodhihirishwa na baadhi ya wahusika kujihusisha na ukahaba pamoja na ufisadi. Mhusika mkuu ni Rehema ambaye anapatwa na misukosuko mingi maishani. Misukosuko hii inatokana na baba yake, Fuad, kumuoa mke wa pili, Adila. Tendo hili linabadilisha mahusiano ya kijamii katika kazi hii. Aziza, mke wake wa kwanza, anahamishwa hadi katika shamba la pili la Fuad kule Ramwe. Hatimaye, Aziza aliaga dunia na Rehema akachukuliwa hadi nyumbani mwa Fuad na kupewa kazi za nyumbani. Mashaka ya kimwili na kisaikolojia aliyoyapata Rehema yanamfanya achukue uamuzi wa kutoroka nyumbani. Tunaelezwa:

> Baada ya kifo cha mama yake zaidi ya miaka sita iliyopita, walimchukua mbiju ati kumlea kumbe kuongeza idadi ya watumishi katika jumba lao. Wakati huo alikuwa mdogo,maskini, hana mtu. Walimkabidhi mikononi mwa watumishi, cheo chake, mtumishi wa watumishi. Ufagio ulimfanya suguru mikononi…(uk 22).

Masaibu haya yalimfanya Rehema kupitia hali ngumu ya kisaikolojia iliyotokana na dhihaka na unyanyasaji wa watumishi wa baba yake. Hakuelewa kwa nini abaguliwe ilhali alikuwa mtoto wa Fuad, hata kama mama yake alikuwa ameaga dunia. Jambo lingine ambalo lilimtia uchungu ni ya kwamba ndugu zake wa kambo walipendelewa;Samir alikuwa masomoni Ulaya na Salma mjini akisoma. Hali hizi ngumu alizozipitia ndizo zilimpatia ari ya kuondokea mazingira hayo yaliyomdhalilisha.Tunaelezwa:

> Usiku alipokuwa katika chumba chake kilichokuwa kizuri kidogo tu kuliko vya mayaya, aliota juu ya maisha mema yaliyoko nje ya gereza lile, na kutafakari juu ya njia za kutorokea (uk 22).

Rehema alikuwa amekengeushwa na mazingira yake. Alitamani kuishi kwa Bikiza shoga ya marehemu mama yake ingawaje nyumba yake ilikuwa kijibanda kilichojiinamia. Hata hivyo, ilikuwa wazi jambo hili halingekubaliwa na Baba yake. Mortimer (katika Mugo 2016) Anaeleza kuwa: “Safari ni ziara au mwendo wa kulazimishwa ambapo msafiri anatafuta suluhu ya matatizo yake au uhamisho katika juhudi za kupata makao mapya’’(uk169). Hali hii ndiyo inampata Rehema. Anapania kuyatoroka maisha yake ya dhiki kwa matamanio kuwa atapata afueni anakokusudia kutorekea. Kwa hivyo, bila kumfahamisha yeyote, anatoroka kutoka kwao na kuelekea mjini akipitia msituni. Tajriba anazozipitia Rehema katika utoro wake zinamfungulia msomaji jamii ya mwandishi na kuyaweka mahusiano ya kijamii bayana. Anapotoroka nyumbani anapitia vichakani na hatimaye porini akielekea mjini Mwembe shomari. Anajikwaa na kuanguka chini na kupoteza fahamu. Anapopata fahamu anajipata kwenye kibanda cha Sulubu. Anapitiwa na kipindi cha wasiwasi mkubwa kwa kuhofia kunyanyaswa na mtu huyu asiyemjua. Hatimaye, anatambua kwamba Sulubu ni mtu mwenye utu na heshima. Anamtunza na hatimaye kuandamana naye hadi Mwembeshomri. Walipofika viungani vya mji waliagana na Rehema akamshukuru kwa fadhila zake. Rehema anakutana na Kidawa na baada ya gumzo naye, Kidawa anakubali kuandamana naye siku ya pili hadi Mwembeshomari walikoishi na wenzake wawili, Chiku na Ruzuna. Baada ya kujadiliana, walikubali kumkaribisha Rehema aishi nao.

Wenyeji wa Rehema waliishi maisha ya ukahaba.Hawakutaka kumshirikisha katika uozo huu kwa hivyo walifanya juhudi za kumtafutia kazi. Hatimaye, alipata kazi kwa Mansuri ambaye aliishi katika mtaa wa magorofa mbali na mahali hapo. Mwanzoni, kazi ya uyaya aliyoipata ilimfurahisha kwa kumpa utaji

lakini, hatimaye, Mansuri alimhadaa na kumuingiza kwenye uzinzi ambao karibu ungalisababisha mauti yake. Hii ilikuwa wakati walifumaniwa na mkewe Mansuri kama wamelala pamoja. Rosi mkewe Mansuri alimuadhibu Rehema kwa tendo hilo la usaliti. Hatimaye Rehema aliingilia maisha ya anasa bila kujali. Mwisho yakamchosha na akaanza kuyaona kama ubatili mtupu. Ni wakati huu ambapo Bikiza anatokeza kwake Topea na kumuomba waandamane naye hadi Mbinju kwa babake akagawiwe mali ya marehehemu mama yake.Pendekezo hili linamtia woga lakini hatimaye anakubali na kuandamana na Bikiza hadi Ramwe. Baba yake anakubali kumgawia mali ya marehemu mama yake. Anapewa shamba la Ramwe.

Maisha ya Rehema yanatokea kama safari iliyogubikwa na wingu ambalo linamzuia msomaji kuelewa hatima ya maisha yake. Safari yake ya kwanza ya kujitoma porini ni kama jazanda inayoashiria kuwa kama ilivyo vigumu kuelewa yanayoendelea porini ndivyo ilivyo kitendawili kigumu cha kutegeua au kuelewa mkondo wa maisha ambao ungalichukuliwa na Rehema alipotoroka nyumbani. Vituo tofauti ambavyo Rehema anapitia, katika safari yake vinatuangazia kuhusu jamii husukika. Kituo chake cha kwanza, katika mastakimu ya Sulubu, Sulubu anajidhihirisha kama mtu anayejiheshimu. Anamchukulia Rehema kama bintiye na kumtunza hadi anapopata nafuu. Hatimaye anamuelekeza alikokuwa akielekea.

Kwa kina kidawa tunaona uchochole unawaingiza wahusika katika ukahaba.Pia tunaona ukata unaowafanya kuishi kwenye vibanda ambavyo havina nafasi ya kuwasitiri wanapoendeleza ukahaba wao. Uhayawani unaosababishwa na mfumo wa kikapitalisti ambao unawalazimu watu kutafuta mtaji kwa njia yo yote ile unadhihirika katika nyumba ya kundi hili la makahaba. Kwa Mansuri na Rosi mkewe kuna starehe kidogo.Hakuna msongamano kama katika maeneo ya Topea alikoishi Rehema na wenzake watatu.Lakini pia kuna unyonge wa moyo na adili. Ni katika nyumba yao ambapo Rehema anaparamiwa na kuharibiwa na Mansuri baada ya kuhongwa kwa nguo. Mwishowe, anahamia Ramwe na mumewe Sulubu. Wanaishi maisha ya furaha na utulivu hadi Karim anapotokea na kujaribu kuwapokonya shamba lao, kitendo ambacho kinasababisha mauti ya Karim. Hatimaye wananchi wakishirikiana na jeshi wanipindua serikali kutokana na madhila iliyokuwa ikiwatendea raia.

Kwa kiwango fulani, Sulubu ni mhusika ambaye analazimika kusafiri ili kujitafutia mtaji. Aliishi porini peke yake. Alikuwa anakodisha mashamba ya watu na kufanya kazi ya ukulima ili kujikimu.Wenye mashamba walikuwa hawajali kama msimu nimzuri au la walichokitaka ni kodi ya shamba. Kwa hivyo alikusudia kuhama eneo ambalo alikuwa akiendeleza shughuli zake na kutafuta sehemu nyingine ambayo alitumainia hatadhulumiwa na wenye mashamba.

***b) Kiu***

Riwaya ya *Kiu* inazungumzia aina mbalimbali za kiu zinazodhihirishwa na wahusika. Kiu mbili zinazojitokezakwa uzito kabisa ni kiu ya mapenzi na kiu ya utajiri. Bahati alimpenda sana Idi. Mwinyi pia alimtamani Idi lakini msukumo wake ulikuwa ni kufanya mapenzi naye. Kiu ya utajiri inamfanya Idi kukamia utajiri wa Mwinyi. Ili kuvunja kiu cha wahusika hawa wanalazimika kusafiri. Idi daima yuko safarini kama dereva wa Mwinyi akimpeleka mawindoni alipokuwa akimsaka Bahati. Bahati pia anajikuta safarini akimwendea Idi ili washirikiane katika juhudi za kumhadaa na kumtapeli Mwinyi. Hatimaye Bahati anaangamia anapohadaiwa na Idi wakutane Kinarani ili amkabidhi haki yake. Kwa matumaini makubwa Bahati anasafiri Mnarani kukutana na Idi ili agawiwe ngawira zake lakini anauwawa.

Kwa upande mwingine, babake Bahati alisaka utajirikwakushiriki biasharaya magendo nchini Kongo. Mzee huyu alipoona hawezi kupata utajiri kwao, alifunga safari hadi Kongo ili kushiriki biashara haramu ya pembe za vipusa. Alitumainia kwamba kupitia kwa shughuli hizi angaliweza kuvunja kiu chake cha kutaka kutajirika lakini badala yake alikamatwa kushtakiwa na hatimaye kufungwa gerezani.

***c) Kicheko cha Ushindi***

Katika 'Mji'(katika diwani ya *Kicheko cha Ushindi*), Adam anachoshwa na maisha ya mashambani. Adam anaotesha ndoto ya kutorokea mjini kutokana na maonevu ya wazee wake.Tunaelezwa:

> Kila alipowaza hakukumbuka lini walimsemesha kwa upole, au lini walimuona kachoka. Mikono yake ilikuwa imeota dasi kwa kamba ya kisima, na miguu yake suguru na kovu kwa kutafuta kuni za kupikia mwituni.Tena kulikuwa na kundi la mbuzi la kupeleka malishoni na kulirudisha na konde ya mpunga kuiinga ndege…

Adam anashindwa kuzihimili shida hizi na anaamua kutorokea mjini. Mhusika huyu anachukulia kuwa safari ya kutoka mashambani itampatia uhuru atakapofika anakokwenda kwa rafiki yake Hamadi. Safari yake inapatwa na misukosuko kadhaa. Anapotea baada ya kushukishwa eneo asilolijua na anapompata rafiki yake ingawaje anapokewa vizuri inakuwa bayana hawezi kuishi kwao. Baadaye anapata kazi kwaBabu Miwa (kama waliviomlakabu)ya kusokota gudurumu la kinu ili kukamua miwa. Mfanyikazi mwenzake Kitwana anamwingiza katika genge la wevi ambapo anafanyiwa uhayawani unaomfanya kutoroka na kuachana na kundi hilo. Anapopata kazi kwenye jahazi linalosafiri miji ya mbali anatumainia kujaribu bahati yake hukokwa sababu hana nia ya kurejea kwao tena.

### *d) Uhuru wa Siku moja*

Katika *Uhuru wa Siku Moja,* Mambo anajipata taabani polisi wanapogundua mimea ya bangi shambani mwake na kumtia nguvuni kwa kosa la kupanda bangi. Licha ya juhudi zake za kujitetea anafunguliwa mashtaka na hatimaye kufungwa gerezani. Maisha ya gerezani yanamvunja moyo na kuvuruga maisha yake. Hali hii inamfanya kutamani uhuru alioukuwa nao hapo awali na kwa hivyo anaotesha matumaini ya kutoroka. Anatambua fika kuwa iwapo atapata fursa ya kutoroka basi atalazimika kutekeleza tendo hilo kighafla. Fursa hii inatokea siku moja alipokuwa amepelekwa mbele ya msimamizi wa gereza kuhojiwa na kufahamishwa kuwa ilikuwa imesalia siku moja peke yake amalize kifungo chake. Pindi tu alipotoka kwenye ofisi ya msimamizi aliamua kutoroka.Kwa kuwa hapakuwa na askari karibu alichana mbuga na kuingia machakani. Askari waliokuwa wanashika doria walipiga vipenga na wakatoka shoti kumkimbiza mfungwa. Alipigwa risasi ya mgongoni nakurejeshwa gerezani. Asubuhi yake alipatikana amekufa.

### Hitimisho

Makala haya yamedhihirisha namna M. S. Mohammed alivyotumia kwa ujuzi motifu ya safari kukuza maudhui kwa njia inayofanikisha kazi zake.Kutokana na kazi tulizoteua ni bayana kwamba mwandishi amesawiri matamanio makubwa ya mwanadamu ya kuboresha maisha yake kwa kutafuta uhuru kutokana na hali zinazomtatiza. Hali hizi kama tuliviziona ni kama vile unyanyasaji, na uonevu kama unaofanyiwa Rehema, Sulubu, Adam na Mambo. Uchochole uliowazingira Chiku, Kidawa na Ruzuna uliwavunja moyo wakaona afueni yao ni kutorokea mjini ili waweze kuboresha maisha yao. Kwa upande mwingine mwanadamu pia anaweza kusafiri ili kusaka utajiri. Kichocheo hiki kinaweza kutokana natamaa ya kujitajirisha kwa mfano Idi, na baba ya Rehema. Athari ya motifu katika kazi za M.S. Mohammed ni kusababisha taharuki kwa msomaji. Msomaji anaachwa na maswali mengi kuhusiana na hatima ya wahusika wanaofunga safari. Hawezi kujua vikwazo watazokumbana navyo au kama watatimiza malengo yao. Kwa hivyo mbinu hii inamsaidia mwandishi kuwana kisa chenye msuko unaovutia na pia fursa ya kukuza mandhari anuwai ambamo wahusika wake wanaendeleza shughuli zao. Wahusika wanapitia hatua mbalimbali za ukuaji kuanzia uzuzu, upevukaji hadi kufikia kiwango cha kuwa majasiri. Kwa hivyo, mbinu hii imetumika kwa njia mwafaka na imeboresha kazi za M. S. Mohammed na kuutambulisha upekee wake kama mwandishi.

## Marejeleo

Conrad, J. (1950). *Heart of Darkness.* New York: Doubleday and Company. Inc.

Dandson, P. (1987). *The Sociology of Literature*. Cambridge: Chadywk Harley.

Goldman, L. (1975). *Towaras a Sociology of the Novel*. London: Tavistock Publication.

Mohammed, S. M. (1972). *Kiu*. Nairobi: Longhorn Publlishers.

Mohammed, S. M. (1976). *Nyota ya Rehema*. Nairobi: Oxford University Press.

Mohammed, S. M. (1978). *Kicheko cha Ushindi*. Nairobi. Shungwaya Publishers.

Mugo, K. G. (2016). Journey motif in David Mulwas *Flee Mama Flee*. Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Muthoni, M. (2014). Uhakiki wa Maudhui na Mtindo katika *Tikitimaji.* Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi(Haijachapishwa).

Semzaba, E. (1999). *Funke bugebuge*. Dar-es –Salaam: Dar -es-Salaam University Press.

Silavwe, M. I. (2016). Mtindo katika riwaya ya *Majaliwa* ya Edwin Semzaba. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Haijachapishwa).

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books

Wellek, R. na Warren, A. (wh). (1978). 'Literature and Society'. *Theory of Literature*: London: Penguin.